



MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA

UWASILISHAJI WA MALALAMIKO YA MATOKEO YA USAILI

Dar es Salaam, 27 Aprili, 2025:

Kufuatia tangazo la matokeo ya usaili wa mchujo wa kuandika lilotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tarehe 26 Aprili, 2025, na ili kuhakikisha kuwa, kila msailiwa anapata haki anayostahili, TRA inapenda kuwafahamisha wasailiwa ambao wana malalamiko au ufafanuzi wowote kuhusiana na matokeo hayo kuwasilisha malalamiko yao kwa njia ya barua kwa Kamishna Mkuu, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ndani ya **siku mbili** kuanzia tarehe **28 hadi 29 Aprili, 2025** wakieleza sababu za malalamiko yao.

Barua hizo ziambatanishwe na **namba ya mtihani ya msailiwa**. Barua hizo zitumwe kupitia barua pepe ya **huduma@tra.go.tz** au **services@tra.go.tz**.

Kwa waombaji waliopo Mkoa wa Dar es Salaam wanaweza kupeleka barua hizo kwenye ofisi ya TRA ya Kituo cha Huduma kwa Mlipa Kodi kilichopo Mtaa wa Samora wakati wa saa za kazi.

“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”

Imetolewa na;

IDARA YA USIMAMIZI WA RASILIMALIWATU NA UTAWALA